MARKETINGLINK TANZANIA LIMITED

VIGEZO NA MASHART YA HUDUMA

Tarehe ya Kuanza Kutumika: **09/ 09/ 2026**
Toleo la Nyaraka: **kwanza**

1. UTANGULIZI

Nyaraka hii inaweka Vigezo na Masharti yanayosimamia utoaji wa huduma na **MarketingLink Tanzania Limited** kwa wateja, washirika, taasisi na mashirika yanayopokea au kuingia katika makubaliano ya kupata huduma kutoka kwa Kampuni ya **MARKETINGLINK TANZANIA LIMITED.**
Masharti haya yataunda msingi wa kisheria na kibiashara wa uhusiano kati ya MarketingLink na Mteja kwa kukubali huduma, kusaini mkataba, kuidhinisha (***Proposal au Quotation***). kutoa Purchase Order, kufanya malipo au kutoa maelekezo ya kuanza utekelezaji wa huduma, Mteja atahesabiwa kuwa amekubaliana na Masharti haya.

Endapo kutatokea kutokuwiana kati ya Masharti haya na masharti ya mkataba maalum uliosainiwa kati ya MarketingLink na Mteja, masharti ya mkataba huo maalum yatapewa uzito kwa kiwango cha kutokuwiana huko.

2. WIGO WA HUDUMA

MarketingLink hutoa huduma za kitaalamu katika maeneo ya ***masoko, mawasiliano, utafiti wa soko, masoko mtandao, kampeni za kimkakati, sherehe (activations, content development, media coordination, business development)*** na huduma nyingine zinazohusiana na mahitaji ya Mteja.

Wigo mahususi wa huduma, matokeo yanayotarajiwa, muda wa utekelezaji, gharama na majukumu ya kila upande vitaainishwa katika Proposal au Mkataba wa Huduma husika.
Hakuna kazi au huduma itakayochukuliwa kuwa sehemu ya wigo uliokubaliwa isipokuwa iwe imeainishwa wazi au kukubaliwa kwa maandishi.

3. MAJUKUMU YA MARKETINGLINK

MarketingLink itatekeleza huduma kwa kuzingatia:

i. viwango vinavyokubalika vya taaluma na uadilifu wa kibiashara
ii. wigo wa kazi uliokubaliwa

iii. ratiba ya utekelezaji iliyokubaliwa kwa kuzingatia utegemezi wa taarifa, maamuzi na idhini kutoka kwa Mteja
iv. maelekezo halali yaliyotolewa na Mteja, na
v. sheria na taratibu za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

MarketingLink itakuwa na mamlaka ya kutumia wataalamu, washauri, wakandarasi au watoa huduma wengine pale ambapo kufanya hivyo ni muhimu au kunaongeza ufanisi wa utekelezaji wa huduma.

4. MAJUKUMU YA MTEJA

Mteja atawajibika:

i. kutoa taarifa sahihi, kamili na kwa wakati
ii. kutoa nyaraka, maudhui, nembo, taarifa za bidhaa/ huduma na nyenzo nyingine zinazohitajika
iii. kutoa maamuzi na idhini kwa wakati unaohitajika

iv. kuhakikisha kuwa taarifa au nyenzo anazozikabidhi kwa MarketingLink zinaweza kutumika kihalali
v. kushirikiana na MarketingLink katika utekelezaji wa kazi, na
vi. kutekeleza wajibu wote wa kifedha kwa mujibu wa makubaliano.

Ucheleweshaji unaotokana na kutokutolewa kwa taarifa, nyenzo, maamuzi au idhini kwa wakati unaweza kusababisha marekebisho ya ratiba ya utekelezaji bila MarketingLink kuwajibishwa kwa ucheleweshaji huo.

5. MALIPO NA GHARAMA

Ada za huduma zitaainishwa katika **Proposal, Quotation, Invoice au Mkataba husika.**
Mteja atawajibika kulipa ndani ya muda uliokubaliwa.

Gharama za wahusika wengine kama vile **media buying, production, venue, usafiri, uchapishaji, teknolojia, talent, influencers** au huduma nyingine za nje zitatambuliwa na kushughulikiwa kwa mujibu wa makubaliano ya kibiashara kati ya pande husika.
MarketingLink inaweza kusitisha au kusogeza mbele utekelezaji wa huduma endapo malipo yaliyokubaliwa yatakuwa hayajafanyika ndani ya muda uliowekwa, bila kuathiri haki nyingine za Kampuni kwa mujibu wa mkataba au sheria.

6. MABADILIKO YA WIGO WA KAZI

Mteja anapotaka kuongeza, kupunguza au kubadilisha wigo wa huduma baada ya kazi kuanza, MarketingLink itafanya tathmini ya athari za mabadiliko hayo katika:

1) Gharama
2) Muda wa utekelezaji
3) Rasilimali
4) Matokeo yaliyokwisha kabidhiwa, na
5) Majukumu ya kila upande.

Mabadiliko yenye athari za kibiashara yanaweza kuhitaji idhini ya maandishi na quotation au Change Order mpya kabla ya utekelezaji.

7. MILIKI HAKI ZA UBUNIFU NA KAZI

Kila upande utaendelea kumiliki **Mali miliki** iliyokuwa chini ya umiliki wake kabla ya kuanza kwa mradi. ***Mbinu, mifumo, frameworks, templates, methodologies, vifaa*** na nyenzo za ndani zinazomilikiwa na MarketingLink vitaendelea kuwa mali ya MarketingLink isipokuwa kama imekubaliwa vinginevyo kwa maandishi.

Baada ya Mteja kukamilisha malipo yote yanayohusika, haki za matumizi ya ***deliverables*** zilizotengenezwa mahsusi kwa ajili ya Mteja zitatolewa kwa kiwango kilichoainishwa katika Proposal au Mkataba husika.

8. USIRI WA TAARIFA

Kila upande utalinda taarifa za siri alizopokea kutoka kwa upande mwingine na kuzitumia kwa madhumuni yanayohusiana na utekelezaji wa makubaliano.

Taarifa za siri zinaweza kujumuisha taarifa za biashara, mikakati, mipango ya masoko, taarifa za kifedha, taarifa za wateja, mbinu za biashara, taarifa za kiufundi na taarifa nyingine zisizo za umma.

Wajibu wa usiri utaendelea hata baada ya kukamilika au kusitishwa kwa huduma, isipokuwa pale ambapo taarifa husika imekuwa ya umma kihalali au sheria inayolazimisha ifichuliwe.

9. ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

MarketingLink itashughulikia taarifa binafsi kwa kuzingatia sheria zinazotumika za ulinzi wa taarifa binafsi nchini Tanzania.

Pale ambapo MarketingLink itashughulikia taarifa binafsi kwa niaba ya Mteja, pande zote zitazingatia majukumu yao husika kama yatakavyoainishwa katika Mkataba, Data Processing Agreement au hati nyingine husika.

Mteja atawajibika kuhakikisha kuwa ana msingi halali wa kukusanya na kukabidhi taarifa binafsi kwa MarketingLink kwa madhumuni yaliyokubaliwa.

10. MATOKEO YA KIBIASHARA

MarketingLink itatumia utaalamu na juhudi zinazofaa katika utekelezaji wa huduma.

isipokuwa pale ambapo matokeo maalum yamehakikishwa wazi kwa maandishi, MarketingLink haitawajibika kwa kuhakikisha kiwango maalum cha mauzo, faida, miongozo, usajili, upatikanaji wa wateja au matokeo mengine ya kibiashara ambayo si sehemu ya makubaliano ya kimaandishi

Matokeo ya kampeni yanaweza kuathiriwa na mambo yaliyo nje ya udhibiti wa MarketingLink, ikiwa ni pamoja na mwenendo wa soko, ushindani, tabia za walaji, mabadiliko ya teknolojia, sera za majukwaa ya kidijitali na maamuzi ya Mteja.

11. WAHUSIKA WA TATU

Pale ambapo utekelezaji wa huduma unahusisha third-party providers, MarketingLink inaweza kufanya uratibu au usimamizi wa huduma hizo kwa mujibu wa makubaliano.

Huduma za third parties zinaweza kuwa chini ya masharti, sera, bei, upatikanaji na viwango vya wahusika hao.

12. KUSITISHA HUDUMA

Huduma zinaweza kusitishwa kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa katika Mkataba wa Huduma husika.

MarketingLink inaweza kusimamisha huduma pale ambapo Mteja:

i. anakiuka masharti muhimu ya makubaliano
ii. anashindwa kutekeleza wajibu wa malipo
iii. anatoa maelekezo yanayokiuka sharia, au
iv. anafanya jambo linaloweza kuleta hatari kubwa ya kisheria, kifedha au reputational kwa MarketingLink.

Kusitishwa kwa huduma hakutaondoa wajibu wowote ambao tayari ulikwishatokea kabla ya tarehe ya kusitishwa.

13. MATUKIO YALIYO NJE YA UWEZO WA PANDE

MarketingLink haitawajibika kwa kushindwa au kuchelewa kutekeleza wajibu pale ambapo hali hiyo imesababishwa na tukio lililo nje ya uwezo wake wa kudhibiti ikiwemo:

i. Majanga
ii. Hitilafu kubwa za miundombinu
iii. Kukatika kwa huduma muhimu
iv. Hatua za Serikali
v. Machafuko
vi. migomo, au

matukio mengine yanayotambulika kisheria.

14. UZINGATIAJI WA SHERIA

MarketingLink na Mteja watazingatia sheria, kanuni na matakwa ya mamlaka husika yanayotumika katika utekelezaji wa huduma.

MarketingLink ina haki ya kukataa au kusitisha utekelezaji wa maelekezo ambayo kwa msingi unaofaa, inaamini yanaweza kuisababisha Kampuni kukiuka sheria au matakwa ya mamlaka husika.

15. MABADILIKO YA MASHARTI

MarketingLink inaweza kufanya marekebisho ya Masharti haya ili kuakisi mabadiliko ya huduma, mifumo ya biashara au matakwa ya kisheria.

Toleo jipya litaanza kutumika kuanzia tarehe iliyoainishwa kwenye nyaraka iliyorekebishwa.

16. SHERIA INAYOTUMIKA NA UTATUZI WA MIGOGORO

Masharti haya yataongozwa na kutafsiriwa kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Pande zote zitajitahidi kwanza kutatua mgogoro wowote kupitia majadiliano ya kirafiki na ya kibiashara.

Iwapo suluhisho halitafikiwa, mgogoro unaweza kuwasilishwa katika chombo cha kisheria au mahakama yenye mamlaka kwa mujibu wa sheria.

17. MAWASILIANO RASMI

Maswali, taarifa au mawasiliano yanayohusiana na Masharti haya yawasilishwe kupitia:

MARKETINGLINK TANZANIA LIMITED

Barua pepe: info@marketinglink.co.tz
Simu: +255722 577 809
Tovuti: www.marketinglink.co.tz

© MarketingLink Tanzania Limited.

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA.